




Kutumia kilimo hai katika kilimo cha ndizi kunachangia katika uzalishaji endelevu na udhibiti wa magonjwa na wadudu na huweza kuleta mavuno mengi

Kulingana na Shirikisho la kimataifa la harakati za kilimo hai (IFOAM, 2008), Kilimo-hai kinafafanuliwa kuwa ni “ mfumo wa uzalishaji ambao unaendeleza afya ya udongo, mifumo ya ikolojia na watu. Kilimo hiki hutegemea kwenye michakato ya ki-ikolojia, bioanuwai na mizunguko asilia ambayo inakubaliana na mazingira ya maeneo husika, badala ya kuingiza pembejeo ambao zina athari mbaya. Kilimo hai kinajumuisha utamaduni, ubunifu na sayansi ili kunufaisha mazingira tunayoshirikiana na kukuza mahusiano ya haki na maisha bora kwa wote wanaohusika”.

Utaratibu wa usimamizi wa bustani ya ndizi



Usimamizi sahihi huimarisha mimea na hupunguza kuenea kwa wadudu na magonjwa.

- > Weka mazalia 3 hadi 4 kwa shina
- > Ondoa majani ya zamani kwani yanaficha magonjwa.
- > Acha majani 8 hadi 10 wakati mgomba unabeba, na 4 wakati wa kuvuna.
- > Tumia majani yaliyoondolewa kama matandazo.
- > Ondoa machipukizi dume ili kupunguza kuenea kwa ugonjwa.

Udhibiti wa magonjwa na wadudu



1. Tumia vifaa safi vya kupandia kwa ajili ya kuanzisha bustani mpya.

2. Ongeza mboji katika mashimo ya kupandia, weka mbolea ya kilimo hai juu na weka mabaki ya shamba kama matandazo.



3. Safisha vyombo na viatu au miguu kabla ya kuingia shamba lisilo na ugonjwa.



4. Bustani zilizoshambuliwa sana na magonjwa zifyekwe na kupandwa zao jingine.

Kilimo hai kinasisitiza kuzuia maambukizi na kuenea kwa wadudu na magonjwa.

- > Tumia aina zinazohimili magonjwa.
- > Tumia vifaa safi kwa ajili ya kupanda
- > Hakikisha usafi wa shamba.
- > Eneo kuzunguka shina lisiwe na kitu chochote.
- > Ongeza rutuba ya udongo.
- > Haribu mashamba yaliyojaa ugonjwa na usipande ndizi kwa mwaka 1 hadi 2.

Kuboresha rutuba ya udongo



Ongeza mboji kwenye shimo la kupandia



Mara kwa mara weka mboji na panda mazao yanayofunika ardhi



Weka matandazo au panda mazao ya kufunika ardhi


Hifadhi ya udongo na maji

- > Jenga uzio na panda mazao ya kufunika ardhi kuzuia maji kupotea na mmomonyoko wa udongo
- > Tumia miti ya kivuli na matandazo kuhifadhi unyevu wa udongo.


Mbolea za kilimo hai

- > Tumia mboji katika kupanda miche kwenye mashimo.
- > Ongeza mbolea kwa juu kabla tu ya kuchanua


Kilimo mseto cha ndizi na udhibiti wa magugu



Ndizi vichaka vya miti jamii ya mikunde
Miti Mazao ya kila mwaka



Ndizi Kahawa/mti wa matunda
Mazao ya kila mwaka



Ndizi Miti ya kuzuia upepo
Miti

Mfumo wa ghorofa

Ghorofa ya juu

- > Tumia miti ya kivuli kukinga dhidi ya upepo na kuzalisha mbao

Ghorofa ya kati

- > Panda miti ya matunda, kakao na kahawa kushamirisha uzalishaji wa ndizi.

Ghorofa ya chini

- > Panda mazao ya kila mwaka na mazao ya mikunde yanayofunika udongo
- > Kupalilia kwa muda stahiki huondoa ushindani wa magugu na magonjwa.

Utunzaji sahihi baada ya kuvuna na upatikanaji wa soko



Hakikisha mikungu haianguki ardhini

Ndizi zilizovunwa zishughulikiwe kwa uangalifu



Mikungu iliyovunwa iwekwe kwenye kivuli na isilundikwe pamoja

- > Hifadhi sahihi baada ya kuvuna huzuia ubora kupungua.
- > Mazao bora ya kilimo hai yana soko kubwa nje ya nchi.
- > Shirikianeni na wakulima wengine kupunguza gharama za uthibitisho.

